**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAJI**

# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI TABORA (TUWASA)

**S.L.P 147, TABORA**

Barua pepe: ***maji@tuwasa.go.tz; md@tuwasa.go.tz***

**ZIARA YA KAMATI YA SIASA YA CHAMA CHA MAPINDUZI WILAYA YA TABORA**
**22.03.2024**

# TAARIFA FUPI YA HUDUMA YA MAJI KATIKA MANISPAA YA TABORA NA MIJI YA SIKONGE, URAMBO, UYUI (ISIKIZYA) NA KALIUA.

**MACHI, 2024**

## 1.0 MAELEZO YA HUDUMA KWA UFUPI

*TUWASA* ni kifupi cha maneno *"Tabora Urban Water supply and Sanitation Authority"* ambayo ina jukumu la kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwenye Manispaa ya Tabora pamoja na Miji ya Sikonge, Urambo, Uyui (Isikizya) na Kaliua.

### 1.1 Huduma ya Majisafi

i. Chanzo cha maji kwa Mji wa Tabora ni Bwawa la Igombe na Ziwa Victoria ambavyo vyote vina uwezo wa kuzalisha maji jumla ya **lita 57,842,000** kwa siku. Maji hayo yanatosheleza mahitaji ya Manispaa ya Tabora hadi mwaka 2045 (WAPCOS, 2015). Bwawa la Igombe pekee lina uwezo wa kuzalisha **lita 30,000,000** kwa siku na miundombinu ya Ziwa Viktoria imesanifiwa kuleta maji Tabora Manispaa **lita 27,842,000** kwa siku.

ii. Mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Tabora ni lita 35,130,000 kwa siku ikijumuisha Miji ya Urambo, Sikonge, Uyui (Isikizya) na Kaliua. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa mitandao ya mabomba kwenye Miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua na kutokuwepo maji ya kutosha kwenye maeneo hayo, uzalishaji halisi wa maji kwa sasa ni lita 19,500,000 tu kwa siku.


iii. Upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Tabora na Mji wa Isikizya (Makao makuu ya Wilaya ya Uyui) imefikia 95%. Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge ni 40.5%, Urambo ni 24.5% na Kaliua ni 26%. Maeneo ya Urambo, Sikonge na Kaliua yapo kwenye mradi wa Miji 28 ambao utekelezaji wake umeanza mwezi Aprili, 2023 na umefikia 32% hadi Januari, 2024. Mradi huo umepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2025. Baada ya kukamilika kwa mradi huo, upatikanaji wa maji kwa Miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua utafikia zaidi ya 95%.

iv. Manispaa ina jumla ya Kata 29. Kata 28 zimefikiwa na mtandao wa mabomba na Kata 1 ya Ikomwa iko kwenye mradi wa *quick win* ambao unaendelea. Awali, ulipangwa kukamilika mwezi mwezi Machi, 2024 lakini kutokana na kuchelewa kwa malipo, mradi huo umeongezwa muda hadi Juni, 2024.

v. Upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Tabora ni wastani saa 22 kila siku, na Miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua inapata maji kwa wastani wa saa 7 hadi 9 kwa siku.


vi. TUWASA ina jumla ya wateja 35,485 (Februari, 2024) na *unit* moja (lita 1,000 au ndoo 50 za lita 20 kila moja) ya maji inauzwa kwa shilingi 1,950 tangu mwezi Machi, 2022.

vii. Urefu wa mtandao wa Maji umefikia kilomita 1.288.2 kwenye maeneo yote ya utendaji ya TUWASA. Aidha, uwezo wa kuhifadhi maji ni mita za ujazo 24,490.




## 1.2 Huduma ya Majitaka

i. TUWASA ina mfumo wa uondoshaji wa Majitaka wenye urefu wa kilomita 24.74 ambao unahudumia takribani 8% ya wakaazi wa Manispaa. Kuna jumla ya maunganisho (*connections*) 521 ambapo wateja wamegawanyika kwenye makundi ya Majumbani, Biashara, Taasisi na Viwanda kama inavyoonekana kwenye *pie chart* hapa chini.



ii. Kuna Mabwawa manne ya kutibu majitaka ambayo ufanisi wake siyo mzuri kwa sababu ya usanifu wake.

### 1.3 Mauzo, Makusanyo na matumizi

(i) Kwa muda wa miezi saba (7) ya mwaka wa fedha 2023/2024, kumekuwa na Wastani wa mauzo wa shilingi 883mil/- na makusanyo ya Wastani wa shilingi 718mil/- kwa mwezi. Hii ni sawa na 84% ya malengo ya bajeti. Aidha, Matumizi pia yamekuwa ni wastani wa shilingi 718mil/- au zaidi kwa mwezi.

(ii) Upotevu wa maji ni wastani wa 25.29%

## 2.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

### 2.1 MAFANIKIO

(i) Kutoa huduma bora ya majisafi, salama na ya kutosheleza kwa wateja wote wa Manispaa ya Tabora

(ii) Kulipa mishahara ya watumishi kila tarehe 25 ya kila mwezi tangu mwezi Aprili, 2022

(iii) Kuongeza morali ya watumishi na kuwaweka nadhifu kwa kuwa na sare (uniforms) kwa kila siku ya kazi

(iv) Kupata hati safi (unqualified opinion) kutokana na ukaguzi wa CAG kwa miaka ya 2021/2022 na 2022/2023

(v) Kulipa gharama za umeme zinazofikia shilingi 80mil hadi 100mil kwa mwezi

(vi) Kulipa gharama za maji ya jumla kutoka KASHWASA zinazofikia shilingi milioni 100 hadi 250 kwa mwezi

(vii) Kuendelea kupunguza madeni ya wazabuni, mifuko ya jamii na watoa huduma mbalimbali

(viii) Kuongeza mapato ya kila mwezi kutoka wastani wa shilingi 400mil (2021/2022) hadi kufikia wastani wa shilingi 700mil (2023/2024)

(ix) Kusimamia utekelezaji wa miradi na kuikamilisha kwa ubora unaotakiwa

(x) Kuboresha mahusiano na Taasisi mbalimbali zilizopo mkoa wa Tabora

### 2.2 CHANGAMOTO NA MIPANGO YA UTATUZI WAKE

| Na | Changamoto | Utatuzi wa Changamoto |
|---|---|---|
| 1 | Upungufu wa maji kwenye Miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua | Utekelezaji wa mradi wa Miji 28 ambao umeanza na umefikia 34%. Mradi |

| | | |
|---|---|---|
| | | umepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2025 |
| **2** | Wizi wa Mita na *standpipes* kwa wateja | Kufanya msako kwa wauzaji wa vyuma chakavu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Polisi, Usalama na Manispaa ya Tabora. Msako ulifanyika tarehe 13.04.2023 |
| **3** | Upungufu wa usafiri kutokana na ongezeko la maeneo ya kufanyia kazi | TUWASA imetenga shs 250mil/- katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa ajili ya kununua gari moja na Bajaji |
| **4** | Madeni ya kudai kwenye Taasisi za Serikali, hasa JWTZ. Jumla ya shilingi 4.1Bil/- zinadaiwa na TUWASA. | Kufuatilia madeni hayo makao makuu ya Taasisi husika. Mwezi Mei, 2023, JWTZ walilipa jumla ya shilingi 813mil. Tunatarajia kuwa Mwaka huu 2024 watalipa tena. |
| **5** | Madeni makubwa ya kudaiwa. TUWASA inadaiwa na KASHWASA, mifuko ya hifadhi ya jamii, TRA, EWURA na Wazabuni wengine jumla ya shilingi Bilioni 7.4 | TUWASA imeingia makubaliano na baadhi ya wadai ili kulipa taratibu kulingana na makusanyo yake. |
| **6** | Ufinyu wa mtandao wa Majitaka katika Manispaa ya Tabora. Mtandao uliopo unahudumia 8% tu ya Wakazi wa Manispaa. | Wizara ya Maji kwa kushirikiana na TUWASA chini ya mradi wa Usanifu wa mtandao wa Majitaka kwa miji 10 ya Tanzania bara, imeingia mkataba na Mtaalam Mshauri *Luptan consults* wa Dar Es Salaam kwa ajili ya Kufanya Usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni vya ujenzi wa Mradi wa Majitaka katika Manispaa ya Tabora. Mtaalam mshauri anafanya kazi kwa miezi tisa (9) tangu mwezi Juni, 2023 hadi Machi, 2024. |
| **7** | Kutokuwa na Bomba la kusafirisha maji kutoka Bwawa la Igombe kwenda tanki la Itumba ambalo linahudumia maeneo mengi yaliyopo kwenye miinuko pamoja na Kata za pembezoni ambazo ni Uyui, Mtendeni, Kakola, Ikomwa, Ifucha, Itonjanda, Ndevelwa na Ntalikwa. Hali hiyo inasababisha maeneo tajwa kukosa maji pale kunapokuwa na ukosefu wa Maji ya ziwa viktoria. | Wizara ya Maji na TUWASA vipo kwenye hatua ya manunuzi ya Mkandarasi ambaye atatekeleza mradi wa kulaza bomba la kusafirisha maji kutoka Bwawa la Igombe Kwenda Tanki la Itumba ili kuwezesha maji ya Igombe kusambazwa kwenye Kata zote 29 za Manispaa ya Tabora. |

## 3.0 MIRADI INAYOTEKELEZWA NA ILIYOKAMILIKA KWA KIPINDI CHA 2021 HADI 2024

### 3.1. MIRADI YA UVIKO – 19

TUWASA ilipokea jumla ya **shilingi milioni 547** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi katika Manispaa ya Tabora.

Maeneo yaliyohusika na mradhi huu ni Kidatu (mitaa ya Rada na Kidatu B), Malolo (mitaa ya Chang'ombe, Mawiti na Mtakuja), Misha (mitaa ya Ufugajini, Kilumbo na Utusini), Ikindwa na Ulamba. Utekelezaji wa miradi yote ulikamilika kwa 100% mwezi Juni, 2022 na Wananchi wa maeneo husika wanapata maji vizuri.

### 3.2. MIRADI YA *QUICK WIN*

Miradi hii inagharamiwa na Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa juma la **shilingi Bilioni 1.86.** Mikataba ya miradi hiyo ilisainiwa tarehe 16.05.2022 mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora. Wakandarasi tayari wapo uwandani wakitekeleza miradi hiyo na watakamilisha mwezi Desemba, 2023. Miradi hiyo inatekelezwa kwenye maeneo ya Kaliua, Sikonge, Isikizya na Tabora Manispaa kama ifuatavyo: -

| JINA LA MRADI | MKANDARASI | GHARAMA ZA MRADI | MAENEO YANAYOHUSIKA | IDADI YA WATU WATAKA ONUFAIK A | UKAMILI FU WA MRADI (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| *Extension of Water Project at Kaliua* | Kimua *Company Limited*, P.O.BOX 90368, DAR ES SALAAM | 487,531,396 | **Mji wa Kaliua** (Uwanja wa ndege, Kawawa na Kaliua – Mashariki). | 1,100 | 100 |
| *Extension of Water Project at Sikonge* | Kimua *Company Limited,* P.O.BOX 90368, DAR ES SALAAM | 484,844,536 | **Kata za Sikonge** (Sikonge, Mlogolo,Usingilunde na Majengo, na **Kata ya Misheni** (Misheni, Usupilo, Usega, Uyombakuzoba na Mazinge) | 1,750 | 100 |
| *Extension of Water Project at Isikizya* | Jossam and Co. *Ltd*, P.O.BOX 1779, TABORA. | 287,479,093 | Mji wa Isikizya | 800 | 100 |
| *Extension of Water Project at Tabora Municipal* | Kimua *Company Limited,* P.O.BOX 90368, DAR ES SALAAM | 601,868,971 | Kata ya Ntalikwa, tumbi na Ikomwa | 24,205 | 50% |
| **JUMLA** | | **1,861,723,996** | | **27,855** | |

### 3.3. MRADI WA MAJI WA MIJI 28 KWENYE WILAYA ZA SIKONGE, URAMBO NA KALIUA.

Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Kwa upande wa Tabora, Mradi huu unachukua maji ya ziwa Viktoria kutoka Manispaa ya Tabora na kuyapeleka kwenye Makao Makuu ya Wilaya za Sikonge, Urambo na Kaliua. Takribani jumla ya **Dola za Marekani 62,287,420** (takribani shilingi bilioni 143) zitatumika kwa Miji yote mitatu. Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 11 Aprili, 2023, umefikia 34% na utakamilika mwezi Oktoba, 2025 chini ya Mkandarasi Megha Engineering limited na Mhandisi Mshauri WAPCOS, wote kutoka India.

### 3.4 Ujenzi wa Mabwawa ya Majitaka (Sludge ponds)

Ujenzi wa Mabwawa ya kutibu majitaka (Sludge Ponds) unaendelea eneo la Milambo baracks chini ya Mkandarasi *Peritus Exim Private Limited* kwa shilingi Bilioni 1.6.
Mradi umefikia asilimia 35% ya utekelezaji na ulipangwa kukamilika mwezi Machi, 2024 lakini kutokana na kuchelewa kwa malipo na uwepo wa mvua nyingi, mradi huu utakamilika mwezi Julai, 2024

## 4.0 HITIMISHO

Bodi ya TUWASA, Menejimenti pamoja na Watumishi tunatoa shukrani nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kutekeleza miradi ya maji kwa lengo la kutimiza azma yake ya kumtua ndoo mama kichwani.

Aidha, tunashukuru Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Tabora kwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi hii mara kwa mara ili kuhakikisha inakamilika na kuleta manufaa yaliyokusudiwa.

**::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MWISHO::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::**